

SAUTI YA TSC

TOLEO NA. 68 JARIDA LA TUME YA UTUMISHI WA WALIMU TANZANIA (TSC) OKTOBA 2026

TSC YAADHIMISHA SIKU YA MWALIMU DUNIANI



Mwenyekiti wa TSC, Prof. Masoud Hadi Muruke, akisalimiana na mmoja wa wananchi waliohudhuria maonesho katika Viwanja vya Nyerere Square, Dodoma, ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya Siku ya Mwalimu Duniani.

MAWASILIANO: Katibu, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mtaa wa Mtendeni S.L.P 353, DODOMA
Simu: +255 (26) 2322402-4 Barua Pepe: secretary@tsc.go.tz Tovuti: www.tsc.go.tz

MWALIMU NI NGUZO YA MAENDELEO YA JAMII, TUMTHAMINI NA KUMUUNGA MKONO

Siku ya Mwalimu Duniani ni siku muhimu ya kutambua, kuthamini na kuenzi mchango wa walimu katika kujenga jamii na Taifa. Siku hii inatukumbusha kuwa mwalimu ana nafasi kubwa katika kuwaandaa watoto na vijana kupata maarifa, stadi na maadili yanayowawezesha kuwa raia wema na kuchangia maendeleo ya nchi. Kwa kutambua dhamira hii, ni muhimu jamii nzima kuendelea kumheshimu na kumthamini mwalimu.

Tunawapongeza kwa dhiti walimu wote kwa kazi kubwa na yenye dhamana wanayoifanya kila siku ya kufundisha na kuwaongoza wanafunzi. Kazi ya mwalimu siyo tu kufundisha masomo darasani, bali pia kujenga nidhamu, maadili, ubunifu na kujiamini kwa wanafunzi. Mafanikio ya wanafunzi wengi katika maisha ni matokeo ya juhudi, uvumilivu na kujitolea kwa walimu wao.

Tunatoa pongezi kwa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) kwa kuadhimisha Siku ya Mwalimu Duniani na kuandaa shughuli zinazolenga kuwasogezea walimu na wananchi huduma

mbalimbali ikiwemo elimu. Maadhimisho haya yanatoa fursa kwa Tume kuendelea kuwasikiliza walimu, kueleza huduma zinazotolewa na kuimarisha ushirikiano na wadau wa elimu. Hatua hii ni sehemu muhimu ya kutambua mchango wa mwalimu na kuendelea kuboresha mazingira ya utoaji wa huduma.

Tunapotambua mchango wa mwalimu, ni muhimu pia kuhakikisha anapata huduma bora, kwa wakati na kwa haki. TSC inaendelea kutekeleza wajibu wake wa kusimamia utumishi wa walimu na inahidi kuendelea kuboresha huduma zake ili walimu waendeleo kuwa na utulivu wawapo kazini.

Siku ya Mwalimu Duniani iwe ukumbusho kwa kila mmoja wetu kwamba kumthamini mwalimu ni kuthamini elimu, na kuthamini elimu ni kuwekeza katika maendeleo ya Taifa. Kwa walimu wote Tanzania, tunasema: Hongereni kwa kazi kubwa mnayoifanya ya kujenga kizazi cha sasa na kijacho. TSC itaendelea kushirikiana nanyi na kutoa huduma bora ili kuwawezesha kutekeleza kwa ufanisi dhamana yenu ya kujenga Taifa.

KATUNI



BODI YA UHARIRI

Mwenyekiti

Paulina M. Nkwama

Wajumbe

Revocatus P. Misonge
Mectildis F. Kapinga
Lameck S. Mbeya
Zachary A. Dida
Fatuma I. Muya
Edwin Mgendera
Asha Lubuva

Mhariri Mkuu

Artemony T. Vincent

Mhariri

Adili J. Mhina

Msanifu Kurasa

Lucas G. Ogunde

Wasiliana nasi kwa Simu: +255 756 927 131 & +255 735-255238 Barua Pepe: secretary@tsc.go.tz

Au fika Ofisi ya Mawasiliano, Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mtaa wa Mtendeni, S.L.P 353, DODOMA.



www.tsc.go.tz



Tume ya Utumishi wa Walimu

Na Mwandishi – Dodoma.

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) imeungana na walimu na wadau wa elimu kuadhimisha Siku ya Mwalimu Duniani, inayofanyika kila mwaka Oktoba 5, kwa kutambua mchango wa walimu katika kuelimisha, kulea na kuandaa rasilimali watu kwa maendeleo ya taifa.

Maadhimisho hayo yalianza rasmi Oktoba 1, 2026 jijini Dodoma, ambapo Mwenyekiti wa Tume alifanya mkutano na wanahabari na kueleza malengo na shughuli zilizopangwa katika maadhimisho hayo. Mkutano huo ulitumika kuikumbusha jamii kuhusu umuhimu wa Siku ya Mwalimu Duniani na kueleza hatua zinazochukuliwa katika kuimarisha utumishi wa walimu.

Siku ya Mwalimu Duniani ilianzishwa mwaka 1994 na UNESCO kwa kushirikiana na Shirika la Kazi Duniani (ILO). Huadhimishwa kutambua mchango wa walimu na kuhamasisha mijadala kuhusu hadhi ya taaluma, mazingira ya kazi na changamoto zinazowakabili walimu.

Baada ya ufunguzi, TSC iliendesha maonesho katika viwanja vya Nyerere Square, Dodoma, kwa kushirikiana na wadau wa elimu na utumishi wa umma. Maonesho hayo yalitoa nafasi kwa walimu na wananchi kupata taarifa na huduma kutoka TSC, Ofisi ya Rais–Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Ofisi ya Rais–Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Benki ya CRDB na Damu Salama.

Kupitia maonesho hayo, TSC ilitoa elimu kuhusu misingi ya utumishi wa walimu, ikiwemo sheria, kanuni, taratibu na maadili ya taaluma. Huduma na taarifa hizo zinawasaidia walimu kufahamu haki na wajibu wao na namna ya kufuatilia masuala yao ya kiutumishi. Wananchi pia walipata fursa ya ushauri nasaha na kushiriki katika uchangiaji damu kwa ajili ya kusaidia wenye uhitaji.

Shughuli hizo zilifanyika katika kipindi ambacho TSC inaadhimisha miaka 10 tangu ianze kutekeleza majukumu yake mwaka 2016. Tume imesema katika kipindi hicho imesogeza huduma karibu

TSC YAADHIMISHA SIKU YA MWALIMU DUNIANI



Picha zikionesha matukio wakati wa ziara ya Mwenyekiti wa TSC katika maonesho ya Siku ya Mwalimu Duniani yaliyofanyika katika Viwanja vya Nyerere Square, Dodoma, kuanzia tarehe 1 hadi 5 Oktoba, 2026.

na walimu kupitia ofisi zake katika wilaya 139. Pia imeanzisha Mfumo wa Usimamizi wa Taarifa za Walimu (TSCMIS), unaolenga kurahisisha utoaji na ufuatiliaji wa huduma za kiutumishi.

Tume imeeleza kuwa imeendelea kuimarisha elimu kwa walimu kuhusu sheria na maadili ya kazi, pamoja na kuharakisha ushughulikiaji wa mashauri na rufaa. Hatua hizo zina umuhimu kwa kuwa zinawawezesha

walimu kupata mwongozo na huduma za kiutumishi kwa ukaribu zaidi.

Maadhimisho ya mwaka huu yamebeba kaulimbiu: “Mwalimu ni msingi wa elimu bora, ujuzi na ubunifu katika njia ya kufikia Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050.” Kaulimbiu hiyo inaangazia nafasi ya walimu katika kujenga maarifa na ujuzi unaohitajika ili kufanikisha maendeleo ya taifa.

TSC YAADHIMISHA SIKU YA MWALIMU DUNIANI



Picha mbalimbali zikionesha matukio wakati wa ziara ya Mwenyekiti wa TSC katika maonesho ya Siku ya Mwalimu Duniani yaliyofanyika katika Viwanja vya Nyerere Square, Dodoma, kuanzia tarehe 1 hadi 5 Oktoba, 2026.

MWENYEKITI TSC ATOA TAMKO LA MAADHIMISHO YA SIKU YA MWALIMU DUNIANI



Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Prof. Masoud Hadi Muruke akizungumza na waandishi wa habari tarehe 1 Oktoba, 2026 jijini Dodoma.

Na Mwandishi Wetu – Dodoma

Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Prof. Masoud Hadi Muruke, alitoa tamko la Tume kuelekea maadhimisho ya Siku ya Mwalimu Duniani, akieleza mafanikio yaliyopatikana katika usimamizi wa Utumishi wa Walimu pamoja na hatua mbalimbali zilizochukuliwa na Tume katika kuendelea kuboresha huduma kwa walimu nchini.

Prof. Muruke alisema hayo Oktoba 1, 2026, wakati akizungumza na waandishi wa habari katika mkutano wa waandishi wa habari uliofanyika Dodoma, ikiwa ni sehemu ya

kuelekea kilele cha maadhimisho ya Siku ya Mwalimu Duniani, pamoja na maadhimisho ya miaka 10 ya Tume tangu kuanzishwa kwake.

Alisema maadhimisho ya mwaka huu yalikuwa na umuhimu wa kipekee kwa TSC kwa kuwa yalienda sambamba na kutimiza miaka 10 tangu Tume ilipoanzishwa mwaka 2016, kipindi ambacho Tume iliendelea kutekeleza jukumu lake la kusimamia ajira, utumishi na nidhamu ya walimu katika shule za Serikali Tanzania Bara.

Kwa mujibu wa Prof. Muruke, katika kipindi hicho Tume iliendelea kuimarisha mifumo ya utoaji huduma kwa walimu, ikiwemo matumizi ya mifumo ya kidijitali katika kurahisisha

upatikanaji wa huduma na taarifa zinazohusu Utumishi wa Walimu.

Alieleza kuwa TSC iliendelea kufanya maboresho katika maeneo mbalimbali, ikiwa ni pamoja na usimamizi wa ajira, uhamisho, upandishaji wa vyeo, masuala ya nidhamu na utoaji wa elimu kwa walimu kuhusu sheria, kanuni na taratibu zinazosimamia utumishi wao.

“Katika kipindi cha miaka 10, Tume imejifunza, imefanya maboresho na imeendelea kuimarisha mifumo yake ili kuhakikisha walimu wanapata huduma kwa wakati na kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu,” alisema Prof. Muruke.

Aidha, Mwenyekiti huyo alisisitiza umuhimu wa walimu kutambua nafasi yao katika ujenzi wa Taifa, akieleza kuwa ubora wa elimu na maendeleo ya nchi kwa kiasi kikubwa yanategemea ubora, weledi, uwajibikaji na maadili ya walimu.

Alisema TSC itaendelea kushirikiana na Serikali, walimu, vyama vya walimu, wazazi, wanafunzi na wadau wengine wa elimu katika kuhakikisha mazingira ya utumishi wa walimu yanaendelea kuboreshwa ili kuwawezesha kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

Katika hatua nyingine, Prof. Muruke aliwataka walimu kuendelea kuzingatia sheria, kanuni, taratibu na maadili ya Utumishi wa Umma katika utekelezaji wa majukumu yao, akisisitiza kuwa nidhamu na uwajibikaji ni msingi muhimu wa utoaji wa elimu bora.

Mkutano huo na waandishi wa habari pia ulitoa fursa kwa TSC kueleza shughuli mbalimbali zilizofanyika katika maadhimisho ya Siku ya Mwalimu Duniani, ikiwemo maonesho yaliyofanyika katika Viwanja vya Nyerere Square, Dodoma, kuanzia Oktoba 1 hadi 5, 2026.

Maadhimisho hayo yalitoa fursa kwa TSC na wadau mbalimbali kuwafikia wananchi, kutoa elimu kuhusu huduma zinazotolewa, kueleza mafanikio yaliyopatikana katika kipindi cha miaka 10 ya Tume na kupokea maoni na mrejesho kutoka kwa wananchi na wadau.

Prof. Muruke aliwaalika wananchi, walimu na wadau mbalimbali kushiriki katika shughuli za maadhimisho hayo na kutumia fursa hiyo kupata taarifa na elimu kuhusu huduma zinazotolewa na TSC.

MWENYEKITI TSC ATOA TAMKO LA MAADHIMISHO YA SIKU YA MWALIMU DUNIANI



Baadhi ya viongozi wa Tume ya Utumishi wa Walimu wakiwa kwenye mkutano wa Mwenyekiti wa Tume na waandishi wa habari jijini Dodoma tarehe 1 Oktoba, 2026.

TSC YAFANYA MAPITIO YA KANUNI ZAKE KUBORESHA HUDUMA KATIKA UTUMISHI WA WALIMU



Mkurugenzi wa Kitengo cha Huduma za Sheria Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Wakili Edwin Mgendera, akimwakilisha Katibu wa TSC, akitoa hotuba ya ufunguzi wa kikao kazi cha kupokea maoni kuhusu maboresho ya Kanuni za Tume ya Utumishi wa Walimu za mwaka 2016 tarehe 14, Septemba, 2026 mjini Morogoro.

Na Mwandishi Wetu – Morogoro

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) imeanza mchakato wa mapitio na maboresho ya Kanuni za Tume ya Utumishi wa Walimu za mwaka 2016 kwa lengo la kuimarisha mfumo wa kisheria unaotumika katika kusimamia masuala ya ajira, maendeleo, nidhamu na utendaji wa walimu nchini.

Akizungumza wakati wa ufunguzi wa kikao kazi cha kupokea maoni kuhusu maboresho ya Kanuni

hizo, Mkurugenzi wa Kitengo cha Sheria TSC, Wakili Edwin Mgendera aliyemwakilisha Katibu wa Tume, alisema mapitio hayo ni sehemu ya juhudi za kuhakikisha Sheria na Kanuni zinabaki kuwa nyenzo madhubuti katika utekelezaji wa majukumu ya Tume kwa kuzingatia mahitaji ya sasa.

Alisema baada ya Tume kutekeleza majukumu yake kwa kipindi cha miaka 10, uzoefu uliopatikana umeonesha umuhimu wa kuangalia maeneo mbalimbali ya mfumo wa kisheria na kubaini yale yanayohitaji maboresho.

“Tunahitaji Sheria na Kanuni zinazotusaidia kutekeleza majukumu ya Tume kwa ufanisi zaidi,” alisema Wakili Mgendera.

Aidha, alisisitiza umuhimu wa kuwa na uelewa unaofanana miongoni mwa wadau wanaohusika na utekelezaji wa masuala ya utumishi na nidhamu ya walimu, akieleza kuwa tofauti za uelewa katika ngazi mbalimbali zinaweza kuathiri utekelezaji wa taratibu na hatimaye kuleta changamoto katika utoaji wa huduma.

Kwa upande wake, Mectildis Kapinga, Mkurugenzi Msaidizi wa Sehemu ya Ajira na Maendeleo ya Walimu TSC, aliyemwakilisha Mkurugenzi wa Ajira, Maadili na Maendeleo ya Walimu, alisema uzoefu wa miaka 10 wa Tume umeibua changamoto mbalimbali zinazohitaji kushughulikiwa kupitia maboresho ya Sheria na Kanuni.

Alisema mchakato huo unahitaji ushirikiano wa wadau mbalimbali kwa kuwa kila mshiriki ana nafasi katika kuhudumia walimu, hivyo maoni na uzoefu wao ni muhimu katika kujenga mfumo bora wa utoaji huduma.

Kikao hicho, kimewakutanisha wataalamu wa sheria, rasilimali watu, maadili na maendeleo ya walimu, pamoja na nidhamu na maadili ya walimu kutoka ndani na nje ya TSC.

Kikao hicho kimeleenga kupata maoni ya kitaalamu yatakayosaidia kuhakikisha Kanuni zinazoborishwa zinazingatia misingi ya haki, uwazi, uwajibikaji na ufanisi, huku zikilenga kulinda haki za walimu, kuimarisha nidhamu na kuweka mazingira bora ya utendaji kazi.

Mchakato huo pia unalenga kuhakikisha Kanuni za Tume zinaendana na Sheria ya Utumishi wa Umma pamoja na Kanuni zake za mwaka 2022, ili kuondoa migongano na kuweka uelewano katika utekelezaji wa masuala ya utumishi wa umma.

Kikao kazi hicho kilifanyika kuanzia tarehe 14 hadi 17 Septemba, 2026 katika Ukumbi wa Morogoro Hotel, Morogoro.

TSC YAFANYA MAPITIO YA KANUNI ZAKE KUBOresha HUDUMA KATIKA UTUMISHI WA WALIMU



Mkurugenzi Msaidizi wa Sehemu ya Ajira na Maendeleo ya Walimu TSC, Mw. Mectildis Kapinga akitoa neno la utangulizi wakati wa ufunguzi wa kikao kazi cha kupokea maoni kuhusu maboresho ya Kanuni za Tume ya Utumishi wa Walimu za mwaka 2016 tarehe 14 Septemba, 2026 mjini Morogoro.



Baadhi ya washiriki wa kikao kazi cha kupokea maoni kuhusu maboresho ya Kanuni za Tume ya Utumishi wa Walimu za mwaka 2016 wakifuatilia hotuba ya ufunguzi wa kikao kazi hicho tarehe 14 Septemba, 2026 mjini Morogoro.

TSC YAFANYA MAPITIO YA KANUNI ZAKE KUBOresha HUDUMA KATIKA UTUMISHI WA WALIMU



Baadhi ya washiriki wa kikao kazi cha kupokea maoni kuhusu maboresho ya Kanuni za Tume ya Utumishi wa Walimu za mwaka 2016 wakifuatilia hotuba ya ufunguzi wa kikao kazi hicho tarehe 14 Septemba, 2026 mjini Morogoro.

MWENYEKITI TSC APONGEZA HUDUMA ZITOLEWAZO KATIKA MAONESHU YA SIKU YA MWALIMU DUNIANI

Na Mwandishi wetu – Dodoma.

Mwenye kiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Prof. Masoud Hadi Muruke, amefanya ziara katika mabanda ya maonesho yanayofanyika katika Viwanja vya Nyerere Square, Dodoma, na kujionea huduma mbalimbali zinazotolewa kwa wananchi na wadau katika kuadhimisha Siku ya Mwalimu Duniani.

Prof. Muruke alifanya ziara hiyo leo, Oktoba 1, 2026, akiwa ameambatana na Katibu wa Tume, Mwl. Paulina M. Nkwama, ambapo alitembelea mabanda mbalimbali na kupata maelezo kuhusu huduma, taarifa na elimu inayotolewa kwa wananchi na wadau.

Maonesho hayo yaliyoandaliwa na TSC yanafanyika kuanzia tarehe 1 hadi 5 Oktoba 2026 katika Viwanja vya Nyerere Square, Dodoma, ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya Siku ya Mwalimu Duniani, sambamba na kuadhimisha miaka 10 ya Tume tangu kuanzishwa kwake.

Akizungumza baada ya kutembelea mabanda hayo, Prof. Muruke amepongeza juhudi zinazofanywa na TSC pamoja na taasisi na wadau wanaoshiriki katika maonesho hayo kwa kuhakikisha huduma na taarifa muhimu zinawafikia wananchi kwa urahisi.

Amesisitiza umuhimu wa taasisi za umma kutumia maonesho na majukwaa kama hayo kuwafikia wananchi moja kwa moja, kutoa elimu kuhusu huduma zinazotolewa na kupokea mrejesho wa wananchi kwa lengo la kuendelea kuboresha utoaji wa huduma.

Katika maonesho hayo, TSC inashirikiana na taasisi na wadau mbalimbali, wakiwemo Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF), Watumishi Housing Investment (WHI), Chama cha Walimu Tanzania (CWT) na Benki ya NMB.

Mbali na huduma na elimu inayotolewa kuhusu masuala mbalimbali yanayohusu walimu na wananchi kwa ujumla, maonesho hayo pia yamekuwa na huduma ya uchangiaji damu inayotolewa na



Mwenyekiti wa TSC, Prof. Masoud Hadi Muruke, akifanya ukaguzi wa mabanda ya maonesho katika Viwanja vya Nyerere Square, Dodoma, akiwa ameambatana na Katibu wa Tume, Mwl. Paulina M. Nkwama, wakati wa maadhimisho ya Siku ya Mwalimu Duniani, Oktoba 1, 2026.

Wakala wa Damu Salama, ambapo wananchi wanahamasishwa kujitokeza kuchangia damu na hivyo kusaidia kuokoa maisha ya wenye uhitaji.

Maonesho hayo yanaendelea hadi Oktoba 5, 2026, huku TSC

ikiwakaribisha wananchi na wadau mbalimbali kufika katika Viwanja vya Nyerere Square, Dodoma, kupata huduma, taarifa na elimu kuhusu shughuli na huduma zinazotolewa na Tume pamoja na taasisi washiriki.

MWENYEKITI TSC APONGEZA HUDUMA ZITOLEWAZO KATIKA MAONESHU YA SIKU YA MWALIMU DUNIANI



Mwenyekiti wa TSC, Prof. Masoud Hadi Muruke, akisalimiana na washiriki wa maonesho katika Viwanja vya Nyerere Square, Dodoma, wakati wa ziara yake ya kukagua shughuli za maonesho ya Siku ya Mwalimu Duniani.



Katibu wa TSC, Mwl. Paulina M. Nkwama, akisalimiana na wananchi na wadau waliotembelea mabanda ya maonesho katika Viwanja vya Nyerere Square, Dodoma.



Mwenyekiti wa TSC, Prof. Masoud Hadi Muruke, akisaini kitabu cha wageni katika moja ya mabanda ya maonesho yaliyopo katika Viwanja vya Nyerere Square, Dodoma, wakati wa maadhimisho ya Siku ya Mwalimu Duniani.

MWENYEKITI TSC APONGEZA HUDUMA ZITOLEWAZO KATIKA MAONESHU YA SIKU YA MWALIMU DUNIANI



Katibu wa TSC, Mwl. Paulina M. Nkwama, akisaini kitabu cha wageni wakati wa ziara ya kutembelea mabanda ya maonesho katika Viwanja vya Nyerere Square, Dodoma.



Picha za matukio mbalimbali katika Viwanja vya Nyerere Square, Dodoma, ambapo wananchi na wadau mbalimbali walipatiwa huduma katika maadhimisho ya Siku ya Mwalimu Duniani.

MWENYEKITI TSC APONGEZA HUDUMA ZITOLEWAZO KATIKA MAONESHU YA SIKU YA MWALIMU DUNIANI



Picha za matukio mbalimbali katika Viwanja vya Nyerere Square, Dodoma, ambapo wananchi na wadau mbalimbali walipatiwa huduma katika maadhimisho ya Siku ya Mwalimu Duniani.

MWENYEKITI TSC APONGEZA HUDUMA ZITOLEWAZO KATIKA MAONESHU YA SIKU YA MWALIMU DUNIANI



Picha za matukio mbalimbali katika Viwanja vya Nyerere Square, Dodoma, ambapo wananchi na wadau mbalimbali walipatiwa huduma katika maadhimisho ya Siku ya Mwalimu Duniani.

WALIMU KILOLO WATAKIWA KUWAANDAA WANAFUNZI KUKABILIANA NA USHINDANI KATIKA SOKO LA DUNIA

Na Mwandishi Wetu – Kilolo

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Kilolo imewataka walimu wilayani humo kuhakikisha wanatekeleza majukumu yao ipasavyo kwa kuwaandaa wanafunzi kuwa na maarifa, ujuzi na uwezo wa kukabiliana na ushindani katika soko la dunia.

Wito huo umetolewa na Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Kilolo, Bw. Laiton Ng'amilo, wakati akielezea mafanikio ya miaka 10 ya Tume tangu kuanzishwa kwake mwaka 2016.

Alisema ni wajibu wa walimu kujenga kizazi chenye maarifa, maadili na ujuzi kwa ajili ya Taifa, pamoja na kuwalea wanafunzi kimwili, kiafya, kiakili, kijamii na kiroho ili waweze kuwa raia wenye mchango chanya kwa maendeleo yao na Taifa kwa ujumla.

Bw. Ng'amilo alisema kuwa katika kuhakikisha lengo hilo linafikiwa, Serikali kupitia Tume ya Utumishi wa Walimu imekuwa ikitoa elimu kwa walimu wapya na waliopo kazini kuhusu Sheria, Kanuni, Taratibu, Maadili na wajibu wao kwa mwanafunzi, mwajiri, jamii na viongozi mbalimbali, kwa lengo la kuimarisha utoaji wa

elimu na malezi kwa wanafunzi.

"Kupitia uwezeshwaji wa Serikali, Tume imekuwa na mikakati ya kuhakikisha walimu wanafuata maadili ya utumishi wa umma na taaluma ya ualimu na kulinda heshima na haiba ya taaluma hiyo mbele ya wanafunzi, wazazi na jamii. Mikakati hiyo ni pamoja na kutoa elimu kwa walimu wapya kabla hawajapangiwa vituo vya kazi kuhusu maadili na haiba ya ualimu, pamoja na kuwatembelea walimu katika vituo vyao vya kazi na kutoa elimu kuhusu haiba na maadili ya kazi ya ualimu," alisisitiza.

MIONGOZO YAIMARISHA UFAHAMU WA SHERIA NA TARATIBU

Bw. Ng'amilo aliongeza kuwa katika kuwakumbusha walimu kuhusu wajibu wao, Serikali kupitia Tume imeandaa miongozo na machapisho mbalimbali, ikiwemo Mwongozo kuhusu Masuala ya Ajira na Maendeleo ya Walimu, Mwongozo wa Mafunzo Elekezi kwa Walimu Wapya Wanaojiriwa katika Utumishi wa Umma Tanzania Bara na Mwongozo wa Usimamizi wa Maadili na Nidhamu Ngazi ya Shule.

Alisema miongozo hiyo imewasaidia walimu kujenga uelewa kuhusu Sheria, Kanuni na Taratibu zinazosimamia utumishi wao, na hivyo

kuwawezesha kutekeleza majukumu yao kwa kuzingatia maadili ya utumishi wa umma na taaluma ya ualimu.

TSC YABORESHA USIMAMIZI WA AJIRA NA NIDHAMU

Katika hatua nyingine, Kaimu Katibu Msaidizi huyo alisema kuwa kuanzishwa kwa Tume mwaka 2016 kumesaidia kuboresha usimamizi wa ajira, nidhamu, maadili na maendeleo ya walimu, ikiwa ni pamoja na kuwafanya Wakuu wa Shule kuwa mamlaka za nidhamu katika ngazi ya shule na Tume ngazi ya Wilaya kuwa mamlaka ya rufaa.

Alisema hatua nyingine ni kuboreshwa kwa mfumo wa utoaji ajira kwa walimu na kupungua kwa changamoto ya walimu kurejea kazini mara baada ya kumaliza muda wa kutumikia adhabu.

"Ukiangalia safari kutoka UTS mwaka 1962 hadi kuanzishwa TSC mwaka 2016, mafanikio makubwa ambayo Tume imeyapata ni pamoja na kuboresha mfumo wa utoaji wa ajira, kuwafanya Wakuu wa Shule kuwa mamlaka za nidhamu kwa walimu katika ngazi ya shule, Tume ngazi ya Wilaya kuwa mamlaka ya nidhamu na rufaa katika ngazi ya Wilaya, pamoja na uboreshaji wa Kanuni za Maadili ya Kazi ya Ualimu," alisema.

TSC KILOLO YATEKELEZA DIRA YA MAENDELEO 2050

Wakati huo huo, Bw. Ng'amilo alisema kuwa TSC Wilaya ya Kilolo, katika kutekeleza Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050, itaendelea kutoa elimu kwa walimu kuhusu namna ya kuwaandaa wanafunzi wenye maarifa, ujuzi, maadili na uwezo unaohitajika ili kufikia malengo ya Dira hiyo.

Alisema Tume itaendelea kuwahamasisha walimu kujiendeleza kielimu na kitaaluma ili waweze kuendana na mabadiliko ya sayansi na teknolojia.

Aidha, Bw. Ng'amilo aliomba Serikali kuendelea kuiwezesha Tume kutoa mafunzo ya kuwajengea uwezo walimu ili wawe na weledi, maadili na uwajibikaji, pamoja na uwezo wa kutumia kwa ufanisi Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) katika ufundishaji na ujifunzaji.



Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Kilolo, Bw. Laiton Ng'amilo, akielezea mafanikio ya miaka 10 ya Tume tangu kuanzishwa kwake mwaka 2016.

**WALIMU KILOLO WATAKIWA KUWAANDAA WANAFUNZI
KUKABILIANA NA USHINDANI KATIKA SOKO LA DUNIA**

Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Kilolo, Bw. Laiton Ng'amilo, akielezea mafanikio ya miaka 10 ya Tume tangu kuanzishwa kwake mwaka 2016.

WASHIRIKI WA KIKAO KAZI CHA KUPOKEA MAONI KUHUSU MABORESHO YA KANUNI ZA TUME YA UTUMISHI WA WALIMU WAENDELEA NA KIKAO

Na Mwandishi Wetu – Morogoro

Mchakato wa mapitio na maboresho ya Kanuni za Tume ya Utumishi wa Walimu za mwaka 2016 umeendelea kwa hatua ya majadiliano ya kitaalamu, ambapo washiriki wa kikao kazi hicho wamegawanyika katika makundi mbalimbali kwa ajili ya kupitia kanuni hizo na kutoa mapendekezo ya maboresho.

Katika hatua hiyo, washiriki wanachambua vifungu mbalimbali vya Kanuni hizo kwa kuzingatia uzoefu wa utekelezaji wa majukumu ya Tume pamoja na mahitaji yaliyopo katika utoaji wa huduma za utumishi wa walimu.

Majadiliano hayo yanatoa fursa kwa wataalamu kutoka maeneo mbalimbali kubadilishana uzoefu na mitazamo kuhusu namna Kanuni hizo zinavyoweza kuboreshwa ili ziweze kusaidia katika utekelezaji wa majukumu ya Tume kwa ufanisi zaidi.

Washiriki hao wanatoka katika maeneo mbalimbali ya kitaalamu, wakiwemo wataalamu wa Sheria, Rasilimaliwatu, Ajira na Maendeleo ya Walimu, pamoja na Nidhamu na Maadili ya Walimu, hivyo kutoa nafasi ya kupata maoni yanayozingatia mitazamo mbalimbali ya utekelezaji.

Miongoni mwa maeneo yanayozingatwa katika majadiliano hayo ni namna ya kuhakikisha vifungu vya Kanuni vinaeleweka na kutekelezeka kwa ufanisi katika ngazi mbalimbali zinazohusika na usimamizi wa utumishi wa walimu.

Aidha, washiriki wanatoa mapendekezo kwa kuzingatia changamoto na uzoefu

unaopatikana katika utekelezaji wa majukumu ya Tume, kwa lengo la kusaidia kuboresha mfumo wa kisheria unaosimamia utumishi wa walimu.

Kikao kazi hicho cha siku nne kilifanyika katika Ukumbi wa Morogoro Hotel, Morogoro kilihitimishwa tarehe 17 Septemba 2026.



Washiriki wa kikao kazi cha kufanya mapitio na maboresho ya Kanuni za Tume ya Utumishi wa Walimu za mwaka 2016 wakiwa katika vikundi kujadili na kutoa mapendekezo juu ya maboresho ya kanuni hizo.

WASHIRIKI WA KIKAO KAZI CHA KUPOKEA MAONI KUHUSU MABORESHO YA KANUNI ZA TUME YA UTUMISHI WA WALIMU WAENDELEA NA KIKAO



Washiriki wa kikao kazi cha kufanya mapitio na maboresho ya Kanuni za Tume ya Utumishi wa Walimu za mwaka 2016 wakiwa katika vikukundi kujadili na kutoa mapendekezo juu ya maboresho ya kanuni hizo.

WASHIRIKI WA KIKAO KAZI CHA KUPOKEA MAONI KUHUSU MABORESHO YA KANUNI ZA TUME YA UTUMISHI WA WALIMU WAENDELEA NA KIKAO



Washiriki wa kikao kazi cha kufanya mapitio na maboresho ya Kanuni za Tume ya Utumishi wa Walimu za mwaka 2016 wakiwa katika vikukundi kujadili na kutoa mapendekezo juu ya maboresho ya kanuni hizo.

Na Mwandishi Wetu – Iringa**TSC YASAIIDIA KUSOGEZA HUDUMA
KARIBU NA WALIMU – IRINGA**

Uanzishwaji wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) mwaka 2016 umewezesha walimu kupata huduma kwa urahisi zaidi karibu na mazingira yao ya kazi, sambamba na kujengewa uwezo kuhusu Sheria, Kanuni na Taratibu zinazosimamia utumishi wao.

Kauli hiyo imetolewa hivi karibuni na Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Iringa, Bi. Frida Mwiwula, alipokuwa akielezea mafanikio ya miaka 10 ya Tume tangu kuanzishwa kwake.

Alisema katika kipindi hicho, Tume imeendelea kuwajengea uwezo walimu kuhusu Sheria, Kanuni na Taratibu za utumishi, jambo ambalo limeواسaidia kutekeleza majukumu yao kwa kuzingatia maadili, nidhamu na weledi.

“Kwa kweli safari kutoka Idara ya Utumishi wa Walimu (TSD) hadi kuanzishwa kwa Tume ya Utumishi wa Walimu mwaka 2016 imekuwa ya mafanikio makubwa. Kwa sasa huduma kwa walimu imewafikia moja kwa moja na matatizo yao yanapatiwa ufumbuzi kwa wakati,” alisema.

Bi. Frida alisema pia katika kipindi hicho Serikali imeendelea kuiwezesha TSC katika ngazi ya Wilaya kutoa mafunzo kwa walimu kuhusu maadili, nidhamu na maendeleo yao katika utumishi, hatua ambayo imewasaidia kutambua haki na wajibu wao pamoja na madhara ya kutenda makosa yanayoweza kusababisha mashauri ya kinidhamu.

“Moja ya mikakati tunayotumia ni kutoa elimu kwa walimu wa ngazi zote ili kuufanya utumishi wa walimu uheshimike kwa kuwafafanulia Sheria, Kanuni, Taratibu na miongozo ya kazi na kuwahimiza kufuata taratibu za utumishi wa ualimu,” alisema.

Alisema Tume imejikita katika kusimamia maadili na nidhamu ya walimu ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi na hatimaye kuleta matokeo chanya katika sekta ya elimu.

**TSC YABORESHA HUDUMA
KUPITIA TEHAMA**

Bi. Frida alisema katika kipindi cha miaka 10, TSC imeendelea kutumia mifumo ya TEHAMA kuboresha utoaji wa huduma kwa walimu, ikiwemo masuala ya ajira, taarifa za walimu, nidhamu, mawasiliano na utunzaji wa



Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Iringa, Bi. Frida Mwiwula, akielezea mafanikio ya miaka 10 ya Tume tangu kuanzishwa kwake, hivi karibuni katika Ofisi ya TSC Iringa.

kumbukumbu.

“TSCMIS imeleta mapinduzi makubwa katika usimamizi wa walimu na utunzaji wa taarifa zao. Kwa sasa tumehama kutoka kutunza taarifa kwa njia ya nakala ngumu (hard copy) na kuwezesha taarifa kushughulikiwa kwa njia ya nakala laini (soft copy),” alisema.

Aliongeza kuwa usimamizi wa mashauri ya kinidhamu kwa sasa unafanyika kupitia mfumo wa TSCMIS, jambo ambalo limefanya mchakato huo kuwa mwepesi na wenye ufanisi zaidi.

Bi. Frida aliwataka walimu kuendelea kufanya kazi kwa bidii, maarifanakujiituma, hukuwakitekeleza wajibu wao wa kuwajengea wanafunzi kiakili na kimaadili kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu za utumishi.

Alisema kufanya hivyo kutasaidia kufikia lengo la Taifa la kujenga kizazi

chenye maarifa, maadili na ujuzi unaohitajika katika maendeleo ya nchi.

**TSC IRINGA YALENGA KUJENGA
UWEZO WA WALIMU KUELEKEA
DIRA 2050**

Akizungumzia utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050, Bi. Frida alisema Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Iringa imejipanga kuwaelimisha na kuwajengea uwezo walimu kuhusu maarifa, ujuzi na uwezo unaohitajika katika kuwaandaa wanafunzi kukabiliana na mahitaji ya dunia ya sasa na yajayo.

Alisema Tume itaendelea kutoa elimu na kuandaa semina za kuwajengea walimu uwezo ili kuwawezesha kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi na kuchangia kufanikisha azma ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050.

TSC YAS Aidia Kusogeza Huduma Karibu na Walimu – Iringa



Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Iringa, Bi. Frida Mziwula, akielezea mafanikio ya miaka 10 ya Tume tangu kuanzishwa kwake, hivi karibuni katika Ofisi ya TSC Iringa.



Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Iringa, Bi. Frida Mziwula (kulia), akiwa katika picha ya pamoja na Afisa wa Tume, Bw. Lifingo Mngongo, baada ya kumaliza mahojiano kuhusu mafanikio ya miaka 10 ya Tume tangu kuanzishwa kwake.

Na Mwandishi Wetu – Morogoro

Mchakato wa mapitio na maboresho ya Kanuni za Tume ya Utumishi wa Walimu za mwaka 2016 umeendelea kwa hatua ya kuwasilishwa na kujadiliwa kwa pamoja kwa mapendekezo yaliyotolewa na washiriki katika majadiliano ya vikundi.

Katika hatua hiyo, wawakilishi wa makundi wamewasilisha hoja na mapendekezo yaliyotokana na uchambuzi wa vifungu vya Kanuni

TSC YAENDELEA NA MAPITIO YA KANUNI, MAPENDEKEZO YA VIKUNDI YAWASILISHWA

hizo, huku washiriki wengine wakipata fursa ya kutoa maoni, kuuliza maswali na kutoa ufafanuzi kuhusu maeneo yaliyowasilishwa.

Majadiliano hayo yamelenga kuchambua

yaliyotolewa kwa kuzingatia utekelezaji wa majukumu ya Tume na namna Kanuni zinavyoweza kuboreshwa ili kuwezesha utoaji wa huduma bora zaidi katika utumishi wa walimu nchini.



Kikao kazi cha mapitio na maboresho ya Kanuni za Tume ya Utumishi wa Walimu za mwaka 2016 kikiendelea katika hatua ya uwasilishaji wa maoni.

TSC YAENDELEA NA MAPITIO YA KANUNI, MAPENDEKEZO YA VIKUNDI YAWASILISHWA



Kikao kazi cha mapitio na maboresho ya Kanuni za Tume ya Utumishi wa Walimu za mwaka 2016 kikiendelea katika hatua ya uzwasilishaji wa maoni.

TSC YASOGEZA HUDUMA KARIBU NA WALIMU KAHAMA

Na Mwandishi Wetu – Kahama

Kuanzishwa kwa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) mwaka 2016 kumeleta maboresho makubwa katika usimamizi wa utumishi wa walimu na kusogeza huduma karibu na walimu wa shule za msingi na sekondari za umma Tanzania Bara.

Hayo yameelezwa na Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Kahama, Bw. Marco E. Badehe, wakati akielezea mafanikio ya Tume katika kipindi cha miaka 10 tangu kuanzishwa kwake.

Bw. Badehe alisema kuwa moja ya maeneo ambayo yamepata maboresho makubwa ni matumizi ya teknolojia katika utoaji wa huduma, ambapo shughuli mbalimbali za kiutumishi ambazo awali zilitekelezwa kwa kutumia nyaraka za maandishi sasa zinafanyika kupitia mifumo ya TEHAMA, ikiwemo Mfumo wa Taarifa za Usimamizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSCMIS).

Alisema kabla ya kuanzishwa kwa TSC, wakati walimu walipokuwa wakisimamiwa chini ya Kitengo cha Huduma kwa Walimu (Unified Teaching Service – UTS), usajili wa walimu ulifanyika kwa njia ya maandishi katika vijitabu, hali ambayo ilikuwa ikisababisha changamoto katika utunzaji na upatikanaji wa taarifa.

“Kwa sasa, matumizi ya mifumo ya TEHAMA yameboresha usajili na usimamizi wa taarifa za walimu. Vilevile, changamoto ya ucheleweshaji wa upatikanaji wa barua za ajira imepungua kutokana na maboresho yaliyofanyika kupitia mifumo ya Tume,” alisema.

UGATUZI WABOresha UTOAJI WA HUDUMA

Bw. Badehe alisema mafanikio mengine ni ugatuaji wa huduma na madaraka kutoka ngazi ya Mkoa hadi Wilaya, hatua ambayo imesaidia kupunguza mzigo wa walimu waliokuwa wakilazimika kufuata huduma katika ngazi za juu.

Alisema ugatuaji huo umeenda sambamba na kuboreshwa kwa upatikanaji wa vitendea kazi na usafiri, hali iliyoiwezesha TSC kuwafikia walimu katika vituo vyao vya kazi kwa ufanisi zaidi.

“Wakati wa UTS, Utumishi wa Walimu wa Serikali pamoja na walimu wa sekta binafsi ulihusishwa

katika mfumo mmoja wa huduma, jambo lililosababisha changamoto mbalimbali. Kwa sasa, walimu wa Serikali wanahudumiwa katika mfumo unaolenga mahitaji yao, hivyo kurahisisha na kuharakisha utoaji wa huduma,” alisema.

Alisema maboresho hayo yanaonesha namna kuanzishwa kwa TSC kulivyosaidia kujenga mfumo maalumu wa usimamizi wa utumishi wa walimu unaozingatia mahitaji ya kada hiyo.

ELIMU NA USHAURI WAENDELEA KUIMARISHA NIDHAMU

Akizungumzia usimamizi wa maadili na nidhamu, Bw. Badehe alisema TSC imeweka mikakati ya kuzuia changamoto za kinidhamu kwa kutoa elimu kwa walimu kuhusu Sheria, Kanuni, Taratibu na Maadili yanayosimamia utumishi wao.

Alisema elimu hiyo hutolewa kupitia ziara za TSC shuleni, ambapo walimu hupewa uelewa kuhusu haki na wajibu wao, maadili ya taaluma ya ualimu pamoja na namna ya kukabiliana na changamoto za kiutumishi kwa kuzingatia taratibu zilizowekwa.

Aidha, alisema TSC kwa kushirikiana

na wataalamu kutoka Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji imekuwa ikitoa ushauri na unasihi kwa walimu wanaobainika kuwa na changamoto, kabla hali hizo hazijawa kubwa.

“Katika ziara tulizozifanya katika shule za msingi na sekondari kwa ajili ya kutoa elimu kuhusu masuala ya ajira, maadili na maendeleo ya walimu, jumla ya walimu 1,994 walifikia,” alisema.

Aliongeza kuwa katika kipindi hicho Tume pia imewezesha mafunzo elekezi kwa walimu wapya 344 walioajiriwa katika Utumishi wa Umma kabla ya kuanza majukumu yao, pamoja na kuwajengea uwezo Wakuu wa Shule za Msingi na Sekondari 302 kuhusu usimamizi wa maadili na nidhamu ya walimu.

TSC KAHAMA YAWEKA MKAZO KATIKA DIRA YA MAENDELEO 2050

Akielezea utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050, Bw. Badehe alisema TSC Wilaya ya Kahama imeweka mikakati ya kuwawezesha walimu kuendana na mahitaji ya elimu ya sasa na ya baadaye, hususan katika dunia inayobadilika kwa kasi kutokana na maendeleo ya sayansi na teknolojia.

Alisema moja ya mikakati hiyo



Mwenyekiti wa Kamati ya Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Kahama, Bw. Ephraimu Kaijuko Rwamatunguru, akielezea kuhusu usimamizi wa maadili kwa walimu wa shule za umma.

TSC YASOGEZA HUDUMA KARIBU NA WALIMU KAHAMA

ni kuwahimiza walimu kujiendeleza kielimu na kitaaluma ili kuongeza weledi wao na kuendana na mabadiliko ya sayansi, teknolojia na mahitaji ya soko la ajira.

"Tunawahimiza walimu kujiendeleza kitaaluma ili waweze kuendana na mabadiliko ya sayansi na teknolojia, sambamba na kuzingatia misingi ya haki, wajibu, nidhamu na maadili ya kazi ya ualimu, hususan kwa walimu wapya walioajiriwa," alisema.

Bw. Badehe alisema Tume pia imekuwa ikiwahimiza wadau wa elimu, wakiwemo vyuo vikuu na vyuo vya kati, kusogeza huduma za elimu katika ngazi za Wilaya ili kuwawezesha walimu kujiendeleza bila kulazimika kusafiri umbali mrefu.

Aidha, alisema walimu wamekuwa wakihimiza kujifunza na kutumia TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji ili waweze kukabiliana na mabadiliko ya kiteknolojia na kuwaandaa wanafunzi wenye uwezo wa kuishi na kufanya kazi katika mazingira yanayobadilika kwa kasi.

Alisema Tume pia inawahimiza walimu ambao hawana taaluma ya ualimu kujiendeleza kitaaluma ili

waweze kumudu mbinu na njia bora za ufundishaji na ujifunzaji, hususan katika shule za amali.

"Katika kutekeleza Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050, Tume itaendelea kuweka mkazo katika matumizi ya teknolojia, kuwajengea uwezo walimu na watumishi, kuimarisha ushirikiano na waajiri pamoja na wadau, na kusimamia haki, wajibu, nidhamu na maadili ya kada ya ualimu," alisema.

Alisema hatua hizo zinalenga kuhakikisha walimu wanatekeleza majukumu yao kwa weledi na uadilifu, na hivyo kuchangia katika kuwaandaa wanafunzi wenye maarifa, ujuzi na maadili yatakayowezesha Taifa kufikia malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050.

WALIMU WATAKIWA KUZINGATIA MIIKO NA MAADILI YA TAALUMA

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Kamati ya TSC Wilaya ya Kahama, Bw. Ephraimu Kaijuko Rwamatunguru, aliwataka walimu kutambua nafasi yao muhimu katika kujenga Taifa na kuandaa kizazi chenye maarifa, ujuzi, maadili na uwajibikaji.

Alisema mwalimu anatakiwa

kuzingatia haiba na maadili ya taaluma yake akiwa ndani na nje ya eneo la shule, kwa kutambua kuwa yeye ni mlezi na mwalimu wa wanafunzi kwa kushirikiana na wazazi na jamii.

Bw. Rwamatunguru aliwataka walimu kutekeleza majukumu yao ya kila siku kwa kuzingatia Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo ya Utumishi wa Walimu, pamoja na kujiepusha na vitendo na mienendo inayoweza kuwaingiza katika makosa ya kinidhamu.

"Walimu wanapaswa kuzingatia miiko, maadili na viwango vya taaluma ya ualimu kama inavyostahili kada yao. Kama ilivyo kwa kada nyingine zenye miiko na maadili yake, kama vile madaktari, wahandisi, wanasheria na wauguzi, walimu nao wanapaswa kuheshimu na kuzingatia miiko na maadili mahsusi ya taaluma ya ualimu. Kwa kufanya hivyo, walimu wataendelea kuwa mfano bora kwa wanafunzi na jamii na kuchangia kikamilifu katika ujenzi wa Taifa lenye maarifa, ujuzi, maadili na maendeleo endelevu," alisisitiza.



Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Kahama, Bw. Marco E. Badehe, akielezea mafanikio ya Tume katika kipindi cha miaka 10 tangu kuanzishwa kwake mwaka 2016.



Mwenyekiti wa Kamati ya Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Kahama, Bw. Ephraimu K. Rwamatunguru (kulia), akiwa katika picha ya pamoja na Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume Wilaya ya Kahama, Bw. Marco E. Badehe (wa pili kutoka kulia), pamoja na Maafisa wa Tume, Bi. Nimilwa P. Lucas (katikati), Bi. Dorah M. Makea (wa pili kutoka kushoto) na Bi. Neema J. Mcharo (kushoto).

TSC MUFINDI YAOMBA SOMO LA UZALENDU KUFUNDISHWA KATIKA NGAZI ZOTE ZA ELIMU



Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Mufindi, Bi. Leonia Nduye, akielezea mafanikio ya miaka 10 ya Tume tangu kuanzishwa kwake mwaka 2016, hivi karibuni.

Na Mwandishi Wetu – Mufindi

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Mufindi imependekea kuwepo kwa somo la uzalendo na maadili katika ngazi zote za elimu na kuwa somo hilo liwe la lazima, kwa lengo la kuwajengea wanafunzi na walimu tarajali moyo wa uzalendo na kuwafanya kutanguliza maslahi ya Taifa katika kutekeleza majukumu yao.

Kauli hiyo imetolewa hivi karibuni na Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Mufindi, Bi. Leonia Nduye, alipokuwa akielezea mafanikio ya miaka 10 ya Tume tangu kuanzishwa kwake mwaka 2016.

Alisema kuwepo kwa somo hilo kutasaidia kujenga jamii yenye upendo kwa nchi na utayari wa kujitoa kwa ajili

ya Taifa, kwa kutanguliza maslahi ya Taifa badala ya maslahi binafsi.

Bi. Leonia alisema hatua hiyo pia itawasaidia walimu kutekeleza majukumu yao kwa upendo na weledi, huku wakiweza kuwasaidia wanafunzi wenye tabia na mahitaji mbalimbali kufikia malengo yao na hatimaye kuchangia maendeleo ya Taifa na jamii.

Alisema kupitia mafunzo ya uzalendo na maadili, walimu wataweza kuimarisha uelewa na uzingati wa Sheria, Kanuni, Taratibu na maadili yanayosimamia taaluma ya ualimu, na hivyo kujiepusha na vitendo vinavyoweza kuathiri haiba ya mwalimu kama kioo cha jamii.

Bi. Leonia alisema TSC Wilaya ya Mufindi imekuwa ikitekeleza mikakati mbalimbali ya kuimarisha uzalendo, maadili na nidhamu miongoni mwa

walimu, ikiwemo kutoa elimu kuhusu maadili ya kazi ya ualimu, kuwashauri walimu wenye changamoto na kutoa nasaha pale inapohitajika.

Alisema Tume pia imekuwa ikifanya ziara shuleni na kushiriki katika vikao vya walimu wakuu na wakuu wa shule kwa ajili ya kutoa elimu kuhusu maadili ya kazi ya ualimu, pamoja na kuwaelimisha walimu kuhusu haki, wajibu na mipaka yao kiutumishi.

“Tume inapofanya ziara shuleni hukutana na walimu na kutoa elimu, kisha hukutana na wanafunzi ambao hupata fursa ya kuuliza maswali na kutoa maoni yao. Maoni na changamoto zinazobainishwa hufanyiwa kazi na Tume huendelea kufuatilia mabadiliko yanayotokea,” alisema.

TSC MUFINDI YAENDELEA KUIMARISHA NIDHAMU NA MAADILI

Katika hatua nyingine, Bi. Leonia alisema kuanzishwa kwa TSC mwaka 2016 kumeleta maboresho katika usimamizi wa utumishi wa walimu, ikiwa ni pamoja na kuwafanya Wakuu wa Shule kuwa Mamlaka za Nidhamu na Tume ya Utumishi wa Walimu ngazi ya Wilaya kuwa Mamlaka ya Rufaa, pamoja na kuboreshwa kwa mfumo wa utoaji ajira kwa walimu.

Alisema maboresho hayo pia yamesaidia kupunguza changamoto ya walimu kurejea kazini mara baada ya kumaliza muda wa kutumikia adhabu bila kuzingatia taratibu zinazotakiwa.

TSC MUFINDI YAWEKA MKAZO KATIKA DIRA YA MAENDELEO 2050

Akizungumzia utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050, Bi. Leonia alisema Tume itaendelea kuimarisha nidhamu na maadili ya walimu ili waweze kuwaandaa wanafunzi katika malezi na makuzi bora, pamoja na kutoa elimu na mafunzo yatakayowawezesha kukabiliana na mabadiliko na maendeleo ya kijamii.

Alisema Tume pia itahimiza walimu kujiendeleza kitaaluma ili kwenda sambamba na mabadiliko ya sayansi na teknolojia, kuimarisha matumizi ya TEHAMA na kujifunza zaidi kuhusu elimu mtandao.

Aidha, alisema katika kuhakikisha walimu wanazingatia Sheria, Kanuni na Taratibu za utumishi, TSC imekuwa ikishirikiana na waajiri katika kushughulikia changamoto zinazowakabili walimu pamoja na masuala ya mashauri ya nidhamu.

TSC MUFINDI YAOMBA SOMO LA UZALENDU KUFUNDISHWA KATIKA NGAZI ZOTE ZA ELIMU



Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Mufindi, Bi. Leonia Nduye, akielezea mafanikio ya miaka 10 ya Tume tangu kuanzishwa kwake mwaka 2016, hivi karibuni.



Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Mufindi, Bi. Leonia Nduye (kulia), akiwa katika picha ya pamoja na Afisa wa Tume, Bi. Helena John Mbungu (kushoto), baada ya kuelezea mafanikio ya miaka 10 ya Tume tangu kuanzishwa kwake mwaka 2016.

WALIMU 1,737 SHINYANGA WAJENGEWA UWEZO KUHUSU SHERIA NA MAADILI YA UTUMISHI



Walimu wa Wilaya ya Shinyanga wakipata ufafanuzi kuhusu miongozo ya utendaji kazi inayotolewa na Tume ya Utumishi wa Walimu.

Na Mwandishi Wetu – Shinyanga

Jumla ya walimu 1,737 wa shule za msingi na sekondari katika Wilaya ya Shinyanga wamefikwa na mafunzo kuhusu Sheria, Kanuni, Taratibu na Maadili yanayosimamia utumishi wao katika kipindi cha kuanzia Julai 2023 hadi Juni 2026.

Mafunzo hayo ni sehemu ya jitihada za Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) za kuwajengea uwezo walimu kuhusu wajibu wao kiutumishi, maadili ya taaluma ya ualimu na namna ya kutekeleza majukumu yao kwa kuzingatia Sheria na taratibu za utumishi wa umma.

Akielezea mafanikio hayo, Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Shinyanga, Bi. Valentina Constantine Majembe, alisema kati ya walimu hao, 1,118 ni wa shule za msingi na 619 ni wa shule za sekondari.

Alisema TSC imekuwa ikitoa mafunzo hayo mara kwa mara kwa lengo la kuwasaidia walimu kuelewa wajibu wao na kujiepusha na vitendo vinavyoweza kusababisha tuhuma au makosa ya kinidhamu.

“Lengo la mafunzo haya ni kuwajengea walimu uelewa kuhusu Sheria, Kanuni, Taratibu na Maadili yanayosimamia utumishi wao ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa weledi na kujiepusha na vitendo vinavyoweza kuhatarisha ajira zao,” alisema.

WALIMU WAPYA WAPEWA MIONGOZO YA UTUMISHI

Bi. Valentina alisema pamoja na mafunzo, TSC imekuwa ikitoa miongozo mbalimbali ya utendaji kazi kwa walimu, hususan walimu wapya wanaojiririwa katika Utumishi wa Umma Tanzania Bara.

Alisema miongoni mwa miongozo hiyo ni Mwongozo wa Mafunzo Elekezi kwa Walimu Wapya Walioajiriwa katika Utumishi wa Umma Tanzania Bara, Toleo Namba 1 la mwaka 2025.

“Jumla ya walimu 136 walioajiriwa mwaka 2025 wamepewa mwongozo huo ili kuwasaidia kufahamu vyema utumishi wao na majukumu yanayowahusu,” alisema.

Aidha, alisema TSC kwa kushirikiana na Mafisa kutoka Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji imekuwa ikitoa ushauri na unasihi kwa walimu mmoja mmoja wanaobainika kuwa na changamoto katika kuzingatia maadili ya taaluma ya ualimu.

Alisema hatua hiyo inalenga kuwasaidia walimu kutambua changamoto zao mapema na kuchukua hatua stahiki kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu za kazi.

TSC YAFIKISHA ELIMU YA UTUMISHI KWA WALIMU 700

Bi. Valentina alisema TSC pia imekuwa ikishiriki katika vikao

mbalimbali vya walimu na kutoa elimu kuhusu masuala ya Utumishi wa Umma na Utumishi wa Walimu, ikiwemo Sheria, Kanuni, Taratibu, Miongozo, Haki, Wajibu na mipaka ya kiutumishi.

Alisema katika kipindi cha mwaka 2023/2024 hadi 2025/2026, jumla ya walimu 700 walifikwa kupitia elimu hiyo, ambapo walimu 450 walikuwa kutoka Idara ya Elimu ya Msingi na 250 kutoka Elimu ya Sekondari.

Aliongeza kuwa TSC imeendelea kutoa huduma kwa walimu kwa kuzingatia usawa na haki, bila upendeleo, ikiwemo katika zoezi la upandishaji vyeo ambalo hufanyika kwa kuzingatia miongozo iliyowekwa.

TSC YASOGEZA HUDUMA KUPITIA UGATUZI NA TEHAMA

Akielezea mafanikio ya TSC tangu kuanzishwa kwake, Bi. Valentina alisema kuanzishwa kwa Tume na uwepo wa ofisi katika kila Wilaya Tanzania Bara kumesaidia kusogeza huduma mbalimbali karibu na walimu na vituo vyao vya kazi.

Alisema hali hiyo ni tofauti na ilivyokuwa awali wakati walimu walipokuwa wakipata huduma katika ngazi ya Mkoa, jambo lililowalazimu kusafiri umbali mrefu kufuata huduma za kiutumishi.

“Kuanzishwa kwa Tume kumesaidia kusogeza huduma katika ngazi ya Wilaya, jambo

WALIMU 1,737 SHINYANGA WAJENGEWA UWEZO KUHUSU SHERIA NA MAADILI YA UTUMISHI

lililowawezesha walimu kupata huduma mbalimbali kwa urahisi zaidi, zikiwemo barua za ajira rasmi, kuthibitishwa kazini, kupandishwa vyeo, kubadilishiwa vyeo au kazi na vibali vya kustaafu," alisema.

Aidha, alisema matumizi ya Mfumo wa Taarifa za Usimamizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSCMIS) yameendelea kuboresha utoaji wa huduma, kwa kuwa walimu wanaweza kuwasilisha changamoto zao kupitia mfumo huo na kupata huduma kwa wakati.

Alisema pia miongozo mbalimbali ya kiutendaji imeendelea kurahisisha taratibu za usajili na uthibitishaji wa walimu wapya, pamoja na kuwawezesha walimu kufahamu Sheria, Kanuni na Taratibu zinazosimamia utumishi wao.

Bi. Valentina alisema matumizi ya mifumo hiyo yamesaidia kuharakisha usajili na uthibitishaji wa walimu 274 kwa kuzingatia muda uliowekwa kwa mujibu wa Sheria na Kanuni.

WALIMU 2,112 WAPANDISHWA VYEO

Katika eneo la maendeleo ya walimu, Bi. Valentina alisema jumla ya walimu 2,112 walipandishwa vyeo na kusawazishwa madaraja yao



Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Shinyanga, Bi. Valentina Constantine Majembe, akiendelea na majukumu ya kikazi katika ofisi yake.

kulingana na tarehe na miaka yao ya ajira.

Alisema hatua hiyo ilitekelezwa katika kipindi ambacho Serikali ilitoa vibali maalumu vya mserereko wa madaraja kwa walimu mwaka 2024 na kuendelea kutoa vibali vya upandishaji vyeo mwaka 2025, hatua iliyosaidia kurejesha morali ya kazi kwa walimu wengi.

Aidha, alisema katika kipindi cha

kuanzia Julai 2023 hadi Juni 2026, jumla ya walimu 166 waliojiendeleza kitaaluma walibadilishiwa vyeo au kazi kulingana na elimu waliyopata.

TSC SHINYANGA YAWEKA MKAZO KATIKA DIRA YA MAENDELEO 2050

Akizungumzia utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050, Bi. Valentina alisema TSC Wilaya ya Shinyanga inaendelea kusimamia weledi, nidhamu na ufundishaji bora kwa walimu wa shule za msingi na sekondari za umma, ikiwemo kuimarisha ufundishaji wa masomo ya amali.

Alisema msisitizo huo unalenga kuwawezesha wanafunzi kupata maarifa na ujuzi wa vitendo ambao unaweza kuwasaidia kujiajiri na kushiriki kikamilifu katika shughuli za maendeleo.

Aliongeza kuwa TSC inaendelea kutekeleza majukumu yake ya kusajili walimu, kuwasimamia katika maendeleo ya taaluma na ustawi wao, pamoja na kuhakikisha wanafikia viwango vya utendaji vinavyohitajika katika Taifa lenye uchumi unaotegemea maarifa na ujuzi.

WALIMU WATAKIWA KUWAANDAA WATAALAMU WA TAIFA LA KESHO

Wakati huo huo, Bi. Valentina amewataka walimu kuendelea kusimamia maadili ya taaluma ya ualimu na kuwa mfano wa uadilifu, uzalendo na uwajibikaji kwa wanafunzi, wazazi, jamii na Taifa kwa ujumla.

Aliwataka walimu kukuza maarifa yenye tija kwa wanafunzi kwa kuwasha moto wa udadisi, ubunifu na fikra tunduizi katika ufundishaji wao, ili kuwaandaa wanafunzi wenye uwezo wa kukabiliana na changamoto za sasa na zijazo.

"Walimu wanatakiwa kuandaa Taifa la kesho linalohitaji wataalamu wabunifu, watatuzi wa changamoto na mafundi stadi. Hivyo, wajikite katika ufundishaji wa mitaala iliyoboreshwa kwa lengo la kupunguza utegemezi na kujenga jamii yenye uwezo wa kujitegemea," alisema.



Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Shinyanga, Bi. Valentina Constantine Majembe (kushoto), akiwa katika picha ya pamoja na watumishi wa TSC Wilaya ya Shinyanga, Bi. Agnes Kaji Kapela (kulia), Bw. Emmanuel John Mpini (wa pili kutoka kulia) na Bw. Elimeli Obadia Kabuga (wa pili kutoka kushoto).

TSC KISHAPU YASEMA MFUMO WA TSCMIS UMELETA MAPINDUZI KATIKA KUWAHUDUMIA WALIMU



Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Kishapu, Bw. Paul A. Sheka, akiendelea na majukumu yake ofisini.

Na Mwandishi Wetu – Kishapu

Mfumo wa TSCMIS (Teachers' Service Commission Management Information System) umesaidia Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Kishapu kuboresha utoaji wa huduma kwa walimu, hususan katika usimamizi wa ajira, usajili, nidhamu, maadili na maendeleo ya walimu.

Kauli hiyo imetolewa hivi karibuni na Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Kishapu, Bw. Paul A. Sheka, wakati akielezea mafanikio yaliyopatikana katika kipindi cha miaka 10 tangu kuanzishwa kwa Tume mwaka 2016.

Alisema kuwa matumizi ya mfumo huo yamewezesha huduma mbalimbali za Tume kufanyika kwa njia ya mtandao, ikiwemo usimamizi wa ajira na usajili wa walimu, masuala

ya nidhamu pamoja na upatikanaji wa taarifa mbalimbali za Tume. Aidha, mashauri ya nidhamu yamesajiliwa kupitia mfumo huo, hatua inayorahisisha uchakataji na ufuatiliaji wa mashauri.

Bw. Sheka alisema kuwa kabla ya kuanzishwa kwa TSCMIS, watumishi walilazimika kujaza taarifa kwa kutumia nakala ngumu ambazo zilitumwa Makao Makuu ya Tume na baadaye taarifa hizo kurejeshwa Wilayani, jambo ambalo lilisababisha mlolongo mrefu katika utoaji wa huduma.

"Kwa sasa taarifa za walimu zinajazwa kwa njia ya kielektroniki na mwalimu anaweza kupata nakala ya barua yake akiwa Wilayani. Kupitia mfumo huu, mwalimu pia ananufaika na huduma mbalimbali za Tume kwa urahisi na kwa wakati," alisema.

Aliongeza kuwa mfumo huo umeimarisha pia utunzaji wa

kumbukumbu za walimu, ambapo taarifa zinapohitajika zinaweza kupatikana kwa wakati, tofauti na ilivyokuwa awali ambapo watumishi walilazimika kutafuta majalada ili kupata taarifa za walimu, jambo lililokuwa likichukua muda mrefu.

"Mfumo huu umesaidia kutatua changamoto za walimu kwa wakati na kwa uharaka. Masuala mengi yanachakatwa kupitia TSCMIS, ikiwemo mashauri ya nidhamu, usajili wa walimu na upatikanaji wa barua za kuthibitishwa kazini," alisema.

"Hii ni hatua kubwa ambayo tunaishuhudia katika kipindi cha miaka 10 ya Tume ya Utumishi wa Walimu tangu ilipoanzishwa. Tunaishukuru Serikali kwa kuiwezesha Tume kujenga mfumo huu ambao umeturahisishia sisi na wadau wetu katika kutoa na kupata huduma," alisisitiza.

ZIARA SHULENI ZASAIKIA KUPUNGUZA MASHAURI YA NIDHAMU

Katika hatua nyingine, Bw. Sheka alisema kuwa TSC Wilaya ya Kishapu imeweka utaratibu wa kufanya ziara za kikazi katika shule mbalimbali kwa lengo la kutoa elimu kwa walimu kuhusu Sheria, Kanuni, Taratibu na miongozo inayosimamia utumishi wao, hatua ambayo imesaidia kupunguza mashauri ya kinidhamu.

"Tume inapofanya ziara shuleni huwa inawakumbusha walimu kuhusu Sheria, Kanuni, Taratibu na miongozo mbalimbali inayotolewa na Serikali mara kwa mara kuhusiana na haki na wajibu wa walimu," alisema.

Alisema katika kipindi cha mwaka 2025/2026, TSC Wilaya ya Kishapu ilitembelea walimu 345, ambapo walimu 195 walikuwa wa shule za msingi na 150 wa shule za sekondari. Aidha, katika kipindi hicho Tume ilitembelea shule 16, zikiwemo shule za msingi 11 na sekondari 5.

Kwa mujibu wa Bw. Sheka, ziara hizo ni sehemu ya mikakati ya Tume katika kuimarisha maadili na utendaji wa walimu, ikiwemo kuchapisha na kusambaza miongozo mbalimbali kwa walimu wapya na waliopo kazini, pamoja na kuwakumbusha kutekeleza majukumu yao kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu za Utumishi wa Walimu.

Alisema hatua hizo zimechangia kupunguza mashauri ya kinidhamu, ambapo katika mwaka 2023/2024 kulikuwa na mashauri 5, mwaka 2024/2025 mashauri 3, na mwaka 2025/2026 jumla ya mashauri 3.

Bw. Sheka alisema zoezi hilo pia linalenga kulinda maadili na haiba ya taaluma ya ualimu kwa kutoa

TSC KISHAPU YASEMA MFUMO WA TSCMIS UMELETA MAPINDUZI KATIKA KUWAHUDUMIA WALIMU



Afisa wa Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Kishapu, Bi. Valeria Peter Sindibu, akiendelea na majukumu yake.

elimu kuhusu masuala mbalimbali, ikiwemo uvaaji na muonekano, matumizi ya lugha yanayostahili kati ya mwalimu na mwalimu, mwalimu na mwanafunzi, pamoja na mwalimu na wazazi au jamii inayomzunguka.

"Kwa kuzingatia kuwa mwalimu anatakiwa kuwa mfano wa kuigwa na wote anaowahudumia, katika kipindi cha miaka mitatu kuanzia 2024 hadi 2026, walimu 457 walitembelewa na kukumbushwa maadili ya kazi ya ualimu. Kati yao, 279 walikuwa walimu wa shule za msingi na 178 wa shule za sekondari," alisema.

TSC YASHIRIKI KUBORESHA MAENDELEO YA WALIMU

Aidha, Bw. Sheka alisema TSC kwa kushirikiana na Mwajiri imeendelea kuhakikisha walimu wanaostahili wanapandishwa vyeo kwa wakati. Alisema katika mwaka 2025/2026, jumla ya walimu 295 walipandishwa vyeo, ambapo 225 walikuwa wa shule za msingi na 70 wa shule za sekondari.

Aliongeza kuwa katika kipindi hicho, walimu 53 walibadilishiwa kazi au vyeo baada ya kujiendeleza, ambapo walimu 38 walikuwa wa shule za msingi na 17 wa shule za sekondari.

Akitoa ushuhuda, Mwalimu wa Shule ya Msingi Buduhe, Mwl. Neema

Chabona Charles, alisema suala la upandaji vyeo kwa walimu limekuwa likitekelezwa kwa wakati, tofauti na ilivyokuwa hapo awali.

Alisema hatua za TSC katika kutatua changamoto za walimu kwa

wakati zimeleta faraja na kuongeza morali ya walimu katika kutekeleza majukumu yao kwa bidii na maarifa, jambo ambalo linachangia kuboresha kiwango cha taaluma shuleni.

UTEKELEZAJI WA DIRA YA TAIFA YA MAENDELEO 2050

Akizungumzia utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050, Bw. Sheka alisema TSC imejiandaa kuhakikisha walimu wanapata stahiki zao kwa wakati, ikiwemo kupandishwa vyeo na kulipwa stahiki zinazotokana na mabadiliko ya ajira zao.

Aidha, alisema katika kuwaandaa wanafunzi kukabiliana na ushindani wa dunia, TSC inasisitiza walimu kuzingatia maelekezo yaliyopo katika mtaala mpya, ikiwemo ufundishaji wa masomo ya amali katika shule za msingi na sekondari.

Alisema hadi sasa kuna walimu 17 wa masomo ya amali walio kazini, huku walimu 5 wa shule za msingi wakiwa wamepelekwa vyuoni kwa ajili ya kujiendeleza katika masomo ya amali, hatua inayolenga kuunga mkono utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050.

Naye Mwl. Neema Chabona Charles alisema yuko tayari kujiendeleza kielimu ili kwenda sambamba na mabadiliko ya sayansi na teknolojia na kupata maarifa mapya yatakayomwezesha kuwasaidia wanafunzi katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji.



Mwalimu wa Shule ya Msingi Buduhe, Wilaya ya Kishapu, Mwl. Neema Chabona Charles.

TSC KISHAPU YASEMA MFUMO WA TSCMIS UMELETA MAPINDUZI KATIKA KUWAHUDUMIA WALIMU



Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Kishapu, Bw. Paul A. Sheka, akitoa Mafunzo Elekezi kwa walimu wa ajira mpya hivi karibuni.



Afisa wa Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Kishapu, Bw. Kudra M. Prosper, akitoa Mafunzo Elekezi kwa walimu wa ajira mpya hivi karibuni.



MAWASILIANO: Katibu, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mtaa wa Mtendeni S.L.P 353, DODOMA
Simu: +255 (26) 2322402-4 Barua Pepe: secretary@tsc.go.tz Tovuti: www.tsc.go.tz



www.tsc.go.tz



Tume ya Utumishi wa Walimu